TANGAZO LA SERIKALI NA. 752 la tarehe 23/8/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (USHURU WA HUDUMA) YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 42 la 2014

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma) ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024 na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma) ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga 2014 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 4 kwa kuongeza kanuni ndogo ifuatayo mara baada ya kanuni ndogo ya (2):

"(3) Mlipa kodi mkubwa atakayelipa kwa wakati au ndani ya siku kumi na nne baada ya kufunga hesabu za mwaka atalipa ushuru wa huduma wa asilimia sifuri nukta mbili (0.2%) badala ya asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kwa mauzo ya bidhaa au huduma inayofanyika katika eneo la Halmashauri baada ya kutoa ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa.".

Kufutwa na kuandikwa upya kwa Majedwali

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta Majedwali na kuyaandika upya kama ifuatavyo:

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 3)*

Ushuru wa Mashine za Nafaka

| Na. | Aina ya Biashara | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mashine kubwa | Kusaga, kukoboa, kugrade, kupaki na kuwa na stoo | 1,000,000/= kwa mwaka |
| 2 | Mashine ya kati | Kusaga, kukoboa na kuwa na stoo bila kugrade | 500,000/= kwa mwaka |
| 3 | Mashine za kusaga na kukoboa kibiashara | Kusaga na kukoboa kibiashara bila kuwa na stoo wala kugrade | 300,000/= kwa mwaka |
| 4 | Mashine za mtaani | Kusaga na kukoboa kwa kiwango cha chini mtaani | 60,000/= kwa mwaka |
| 5 | Mashine za kufyatua tofali na kuuza | Kufyatua tofali na kuuza paving, nguzo za uzio, nguzo za urembo na biashara nyingine inayoendana na hiyo | 600,000/= kwa mwaka |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)*

Ushuru wa Huduma kwa vyanzo vingine

| Na. | Aina ya Biashara | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) | Muda wa kulipa |
|---|---|---|---|
| 1 | Gereji au karakana | 300,000/= | Kwa mwaka |
| 2 | Taasisi za mikopo | 300,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Maduka ya vifaa vya ujenzi | 120,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Michezo ya kubashiri | 600,000/= | Kwa mwaka |
| 5 | Maduka ya vipuri vya pikipiki | 120,000/= | Kwa mwaka |
| 6 | Uchomeleaji | 120,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Maeneo ya kuoshea magari | 100,000/= | Kwa mwaka |
| 8 | Biashara ndogondogo | 40,000/= | Kwa mwaka |
| 9 | Biashara za kati | 60,000/= | Kwa mwaka |
| 10 | Biashara kubwa | 120,000/= | Kwa mwaka |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma) ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina: …………………………………..……………
Saini………………………..…………………………..
Wadhifa: …………………………………………………
Tarehe…………………………………………………….

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya shinyanga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano uliofanyika tarehe 23-25/3/2023 Mwaka 2022 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya;-

MWL. ALEXIUS REVOCATUS KAGUNZE
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Manispaa Shinyanga*

MH. ELIAS RAMADHAN MASUMBUKO
*Mstahiki Meya wa Halmashauri*
*ya Manispaa ya Shinyanga*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*